

TAKUKURU YAELIMISHA WAFANYABIASHARA - UMUHIMU WA MATUMIZI SAHIHI YA RISITI ZA EFD

Maafisa wa Kurugenzi ya Elimu kwa Umma TAKUKURU wakielimisha wafanyabiashara na wanunuzi/wananchi kutoka maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam juu ya matumizi sahihi ya risiti/stakabadhi za EFD kulingana na bidhaa iliyouzwa au kununuliwa.

Ni kosa chini ya vifungu vya 22 na 32 vya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya Mwaka 2007, mfanyabiashara na mnunuzi kushirikiana kutoa au kupokea risiti/stakabadhi yenye taarifa zisizo sahihi na zenye lengo la kupotosha.